KUMB: PPR/19 - 11/1

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI KUANZIA JUMATANO, TAREHE 6 NOVEMBA 2019

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 6 Novemba 2019.** Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

(a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya **Dar es Salaam**, zimeongezeka ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 2 Oktoba 2019. Kwa mwezi Novemba 2019, bei za rejareja za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 98/lita (sawa na asilimia 4.67), Shilingi 49/lita (sawa na asilimia 2.31) na Shilingi 62/lita (sawa na asilimia 3.00), mtawalia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 97.48/lita (sawa na asilimia 4.95), Shilingi 48.67/lita (sawa na asilimia 2.45) na Shilingi 61.51/lita (sawa na asilimia 3.18), mtawalia.

(b) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli katika mkoa wa Tanga zimepungua ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 2 Oktoba 2019. Kwa mwezi Novemba 2019, bei za rejareja za Petroli na Dizeli kwa **Mikoa ya Kaskazini** (yaani Tanga, Arusha, Kilimanjaro na Manyara) zimepungua kwa Shilingi 104/lita (sawa na asilimia 4.51) na Shilingi 16/lita (sawa na asilimia 0.73), mtawalia. Aidha, kwa kulinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli na Dizeli zimepungua kwa Shilingi 103.30/lita (sawa na asilimia 4.75) na Shilingi 16.04/lita (sawa na asilimia 0.77), mtawalia.

(c) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli katika mkoa wa Mtwara zimebadilika ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 2 Oktoba 2019. Kwa mwezi Novemba 2019, bei za rejareja za Petroli katika **Mikoa ya Kusini** (yaani Mtwara, Lindi na Ruvuma) zimepungua kwa Shilingi 88/lita (sawa na asilimia 3.80) wakati bei za Dizeli zimeongezeka kwa Shilingi 1/lita (sawa na asilimia 0.05). Aidha, kwa kulinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli zimepungua kwa Shilingi 87.72/lita (sawa na asilimia 4.00) wakati bei za Dizeli zimeongezeka kwa Shilingi 1.00/lita (sawa na asilimia 0.05). *Kwa kuwa hakuna Mafuta ya Taa yaliyopokelewa katika bandari ya Mtwara, wamiliki wa vituo vya mafuta katika mikoa tajwa wanashauriwa kununua mafuta hayo kutoka Dar es Salaam na hivyo bei za rejareja za Mafuta ya Taa kwa mikoa hiyo zinatokana na gharama za mafuta hayo kutokea Dar es Salaam na kusafirishwa hadi mkoa husika*.

(d) Kwa kiasi kikubwa, mabadiliko ya bei za mafuta katika soko la ndani kwa mafuta yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Dar es Salaam yanatokana na kuongezeka kwa gharama za usafirishaji wa mafuta (*BPS premiums*) na kuongezeka kwa bei za mafuta katika soko dunia kama inavyoonekana katika **Jedwali C.** Aidha, kama inavyoonekana katika **Jedwali C** na **Jedwali D,** kwa mafuta yaliyoingia nchini kupitia bandari za Tanga na Mtwara, mabadiliko ya bei za mafuta hayo kwa kiasi kikubwa yanatokana na kushuka kwa gharama za usafirishaji wa mafuta na punguzo la bei za mafuta hayo katika soko la dunia kwa mwezi Septemba 2019

ikilinganishwa na zile za mwezi Julai 2019, zilizokuwa zikitumika tangu shehena ya mwisho kupokelewa katika bandari hizo. ***Ifahamike kuwa, kabla ya toleo hili la bei za mafuta za mwezi Novemba 2019, shehena ya mwisho ya mafuta kupokelewa nchini kupitia Bandari ya Tanga na Mtwara ilikuwa ni mwezi Agosti 2019, ambapo gharama ya mafuta hayo ilikuwa ni bei za mafuta katika soko la dunia za mwezi Julai 2019; wakati kwa bandari ya Dar es Salaam, shehena ya mwisho ya mafuta ilipokelewa mwezi Septemba 2019 ambapo gharama ya mafuta hayo ilikuwa ni bei za mafuta katika soko la dunia za mwezi Agosti 2019. Kutokana na tofauti za vipindi vya uagizaji wa mafuta, ulinganifu wa bei kati ya bandari hizi tatu unakuwa na tofauti***.

(e) EWURA inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.

(f) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.

(g) **Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo zisivuke bei kikomo (*price cap*)** kama ilivyokokotolewa na kanuni (*formula)* iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika **Gazeti la Serikali Na. 163 la mwezi Aprili 2018 na Gazeti la Serikali Na. 269 la mwezi Juni 2018**.

(h) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**

(i) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (*Electronic Fiscal Pump Printers*) na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mauzo ya mafuta ya petroli.

JEDWALI A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta Ya Taa (Shs/Lita)
Dar es Salaam	**2,192**	**2,158**	**2,117**
Arusha	**2,253**	**2,243**	**2,123**
Arumeru (Usa River)	2,253	2,243	2,123
Karatu	2,271	2,261	2,141
Longido	2,264	2,254	2,134
Monduli	2,258	2,249	2,129
Monduli-Makuyuni	2,263	2,253	2,133
Ngorongoro (Loliondo)	2,337	2,328	2,208
Pwani (Kibaha)	**2,196**	**2,163**	**2,122**
Bagamoyo	2,203	2,169	2,129
Chalinze Junction	2,206	2,172	2,132
Chalinze (Msata)	2,210	2,176	2,136
Kibiti	2,212	2,179	2,138
Kisarawe	2,199	2,165	2,125
Mkuranga	2,202	2,168	2,127
Rufiji	2,220	2,186	2,145
Dodoma	**2,251**	**2,217**	**2,176**
Bahi	2,258	2,224	2,184
Chamwino	2,246	2,212	2,172
Chemba	2,277	2,243	2,203
Kondoa	2,284	2,250	2,209
Kongwa	2,248	2,214	2,174
Mpwapwa	2,252	2,218	2,177
Mtera (Makatopora)	2,270	2,236	2,195
Geita	**2,357**	**2,324**	**2,283**
Bukombe	2,346	2,313	2,272
Chato	2,378	2,345	2,304
Mbogwe	2,396	2,362	2,321
Nyang'hwale	2,372	2,339	2,298
Iringa	**2,256**	**2,222**	**2,182**
Ismani	2,261	2,227	2,187
Kilolo	2,260	2,227	2,186
Mufindi (Mafinga)	2,266	2,232	2,192
Kagera (Bukoba)	**2,407**	**2,374**	**2,333**
Biharamulo	2,382	2,348	2,307
Karagwe (Kayanga)	2,424	2,390	2,349
Kyerwa (Ruberwa)	2,430	2,396	2,355
Muleba	2,407	2,374	2,333
Ngara	2,395	2,362	2,321
Misenyi	2,416	2,382	2,341
Katavi (Mpanda)	2,400	2,366	2,326
Mlele (Inyonga)	2,382	2,348	2,307
Mpimbwe (Majimoto)	2,393	2,359	2,318

Tanganyika (Ikola)	2,418	2,384	2,343
Kigoma	**2,423**	**2,390**	**2,349**
Uvinza (Lugufu)	2,436	2,402	2,361
Buhigwe	2,413	2,379	2,338
Kakonko	2,380	2,347	2,306
Kasulu	2,409	2,376	2,335
Kibondo	2,388	2,354	2,313
Kilimanjaro (Moshi)	**2,242**	**2,233**	**2,113**
Hai (Bomang'ombe)	2,245	2,236	2,116
Mwanga	2,235	2,226	2,106
Rombo (Mkuu)	2,259	2,250	2,129
Same	2,229	2,219	2,099
Siha (Sanya Juu)	2,249	2,239	2,119
Lindi	**2,243**	**2,237**	**2,176**
Lindi-Mtama	2,248	2,241	2,194
Kilwa Masoko	2,267	2,261	2,151
Liwale	2,279	2,272	2,197
Nachingwea	2,263	2,257	2,206
Ruangwa	2,269	2,263	2,207
Manyara (Babati)	**2,287**	**2,277**	**2,157**
Hanang (Katesh)	2,297	2,288	2,168
Kiteto (Kibaya)	2,302	2,293	2,172
Mbulu	2,299	2,290	2,170
Simanjiro (Orkasumet)	2,319	2,309	2,189
Mara (Musoma)	**2,371**	**2,337**	**2,296**
Musoma Vijijini (Busekela)	2,411	2,378	2,337
Rorya (Ingirijuu)	2,379	2,346	2,305
Rorya (Shirati)	2,414	2,380	2,340
Bunda	2,362	2,328	2,287
Bunda (Kisorya)	2,371	2,338	2,297
Butiama	2,367	2,334	2,293
Serengeti (Mugumu)	2,416	2,382	2,342
Tarime	2,382	2,348	2,307
Tarime (Kewanja/Nyamongo)	2,386	2,352	2,312
Mbeya	**2,299**	**2,265**	**2,225**
Chunya	2,309	2,275	2,234
Chunya (Makongolosi)	2,323	2,289	2,248
Kyela	2,315	2,281	2,240
Mbarali (Rujewa)	2,283	2,249	2,209
Rungwe (Tukuyu)	2,308	2,274	2,234
Morogoro	**2,217**	**2,183**	**2,142**
Mikumi	2,233	2,199	2,158
Kilombero (Ifakara)	2,255	2,221	2,180
Kilombero (Mlimba)	2,277	2,243	2,203
Kilombero (Mngeta)	2,266	2,233	2,192
Ulanga (Mahenge)	2,265	2,232	2,191
Malinyi	2,276	2,242	2,201
Kilosa	2,235	2,202	2,161

Gairo	2,235	2,202	2,161
Mvomero (Wami Sokoine)	2,227	2,194	2,153
Mvomero (Sanga Sanga)	2,217	2,183	2,142
Turiani	2,242	2,208	2,168
Mtwara	**2,229**	**2,223**	**2,190**
Nanyumbu (Mangaka)	2,266	2,259	2,239
Masasi	2,246	2,239	2,216
Newala	2,250	2,244	2,222
Tandahimba	2,243	2,237	2,215
Nanyamba	2,243	2,237	2,215
Mwanza	**2,342**	**2,308**	**2,268**
Kwimba	2,360	2,326	2,286
Magu	2,350	2,316	2,276
Misungwi	2,337	2,303	2,262
Sengerema	2,375	2,341	2,300
Ukerewe	2,402	2,368	2,327
Njombe	**2,284**	**2,251**	**2,210**
Njombe (Kidegembye)	2,305	2,271	2,231
Ludewa	2,322	2,289	2,248
Makambako	2,277	2,243	2,202
Makete	2,315	2,281	2,241
Wanging'ombe (Igwachanya)	2,282	2,248	2,208
Rukwa (Sumbawanga)	**2,365**	**2,331**	**2,290**
Sumbawanga Rural (Mtowisa)	2,365	2,331	2,290
Kalambo (Matai)	2,372	2,338	2,298
Nkasi (Namanyele)	2,378	2,345	2,304
Ruvuma (Songea)	**2,315**	**2,309**	**2,241**
Mbinga	2,328	2,321	2,275
Namtumbo	2,306	2,300	2,270
Nyasa (Mbamba Bay)	2,353	2,347	2,285
Tunduru	2,280	2,274	2,300
Shinyanga	**2,321**	**2,287**	**2,246**
Kahama	2,335	2,301	2,260
Kishapu	2,349	2,316	2,275
Ushetu (Nyamilangano)	2,352	2,318	2,278
Simiyu (Bariadi)	2,362	2,329	2,288
Busega (Nyashimo)	2,355	2,322	2,281
Itilima (Lagangabilili)	2,365	2,332	2,291
Maswa	2,354	2,320	2,279
Meatu (Mwanhuzi)	2,361	2,327	2,286
Singida	**2,283**	**2,249**	**2,208**
Iramba	2,295	2,261	2,220
Manyoni	2,267	2,233	2,193
Ikungi	2,278	2,244	2,204
Mkalama (Nduguti)	2,307	2,273	2,233
Songwe (Vwawa)	**2,308**	**2,275**	**2,234**
Songwe (Mkwajuni)	2,315	2,281	2,241
Ileje	2,312	2,278	2,238

Momba (Chitete)	2,317	2,284	2,243
Tunduma	2,313	2,279	2,238
Tabora	**2,346**	**2,312**	**2,272**
Igunga	2,300	2,266	2,226
Kaliua	2,365	2,331	2,291
Ulyankulu	2,359	2,326	2,285
Nzega	2,311	2,277	2,236
Sikonge	2,358	2,324	2,284
Urambo	2,359	2,326	2,285
Uyui	2,347	2,313	2,273
Tanga	**2,196**	**2,187**	**2,066**
Handeni	2,217	2,207	2,087
Kilindi	2,232	2,222	2,102
Korogwe	2,208	2,199	2,079
Lushoto	2,217	2,208	2,088
Mkinga (Maramba)	2,203	2,194	2,073
Muheza	2,201	2,191	2,071
Pangani	2,203	2,193	2,073

JEDWALI B: BEI KIKOMO KWA BEI ZA JUMLA

	Petroli (Shs/Lita)	**Dizeli (Shs/Lita)**	**Mafuta ya Taa (Shs/Lita)**
DAR ES SALAAM	**2,068.04**	**2,033.98**	**1,994.08**
TANGA	**2,072.06**	**2,062.29**	**1,943.21**
MTWARA	**2,105.42**	**2,098.91**	**-----**

JEDWALI C: SABABU ZA MABADILIKO YA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA NDANI

BANDARI YA DAR ES SALAAM

	Petroli	**Dizeli**	**Mafuta ya Taa**
Mabadiliko ya Bei za mafuta katika soko la dunia	Ongezeko la Dola 19.298/Tani	Ongezeko la Dola 19.814/Tani	Ongezeko la Dola 17.839/Tani
Mabadiliko ya gharama za usafirishaji (*BPS premiums*)	Ongezeko la Dola 29.556/Tani	Ongezeko la Dola 2.217/Tani	Ongezeko la Dola 4.660/Tani

BANDARI YA TANGA

	Petroli	**Dizeli**	**Mafuta ya Taa**
Mabadiliko ya Bei za mafuta katika soko la dunia	Punguzo la Dola 43.237/Tani	Punguzo la Dola 12.524/Tani	n/a
Mabadiliko ya gharama za usafirishaji (*BPS premiums*)	Punguzo la Dola 3.700/Tani	Punguzo la Dola 3.700/Tani	n/a

BANDARI YA MTWARA

	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Mabadiliko ya Bei za mafuta katika soko la dunia	Punguzo la Dola 43.237/Tani	Punguzo la Dola 12.431/Tani	n/a
Mabadiliko ya gharama za usafirishaji (*BPS premiums*)	Ongezeko la Dola 3.700/Tani	Punguzo la Dola 3.700/Tani	n/a

JEDWALI D: BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA DUNIA ZILIZOTUMIKA KUKOKOTOA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA NDANI

	Bandari	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Mafuta yalipokelewa mwezi wa:	**DSM**	Oktoba 2019	Oktoba 2019	Oktoba 2019
	Tanga	Oktoba 2019	Oktoba 2019	Julai 2019
	Mtwara	Oktoba 2019	Oktoba 2019	n/a
Wastani wa bei za mafuta katika soko la dunia kwa mwezi:	**DSM**	Septemba 2019	Septemba 2019	Septemba 2019
	Tanga	Septemba 2019	Septemba 2019	Juni 2019
	Mtwara	Septemba 2019	Septemba 2019	----
Wastani wa bei za mafuta katika soko la dunia kwa miezi inayoonekana hapo juu inalinganishwa na wastani wa bei za mwezi:	**DSM**	Agosti 2019	Agosti 2019	Agosti 2019
	Tanga	Julai 2019	Julai 2019	Juni 2019
	Mtwara	Julai 2019	Julai 2019	----

Nzinyangwa E. Mchany
KAIMU MKURUGENZI MKUU
EWURA